



1. Je ni mtoto gani wa sauli ambaye Daudi alimwoa?

2. Naamani alienda kujiosha katika mto gani kutakaswa ukoma wake?

3. Katika kabila za Israeli ni kabila gani ulikuwa uzao wa kifalme?

4. Je Daudi alipakwa mafuta mara ngapi na wapi?

5. Je ni mji gani ambao Barnaba na Paulo waliwekewa mikono na kanisa kwa agizo la Bwana?

6. Ni mfalme gani aliye tumia vyombo vya hekaluni kwa anasa Mungu akamwadhibu siku hiyo hiyo?

7. Je ni nabii gani aliye tabiri kutoroka kwa mfalme Sedekia kwa kuuvunja ukuta wa yerusalemu kisha kukamatwa na kupelekwa babeli?

8. Ni nabii gani aliye tabiri kukamatwa kwa paulo na kufungwa miguu na mikono?

9. Je ni Nabii gani aliye tabiri (wakati wa kanisa la kwanza la mitume) ujio wa njaa kubwa kutokea katika dunia nzima katika siku za Klaudio.

10. Je ni nani aliye itabiria Yuda kuwa yeyote atakaye baki hapo Yuda atakufa kwa makali ya upanga na kwa njaa, bali atakaye toka kumtumikia mfalme wa Babeli ataishi?



MTIHANI WA BIBLIA (PART 13) (MASWALI YA BIBLIA)

Mtihani mwema Mjoli wa BWANA.

@NURU YA UPENDO

www.wingulamashahidi.org

0652274252 au 0693036618

01/03/2023

MASAHIHISHO YA MTIHANI LEO

MTIHANI WA BIBLIA (PART 13)

(MASWALI YA BIBLIA)

1. je ni mtoto gani wa sauli ambaye Daudi alimwoa?

Jibu. MIKALI

Soma. 1Samweli 18:27-28

2. Naamani alienda kujiosha katika mto gani kutakaswa ukoma wake?

Jibu. YORDANI

Soma. 2Wafalme 5:10-14



3. Katika kabila za Israeli ni kabila gani ulikuwa uzao wa kifalme?

Jibu. YUDA

Soma. Mwanzo 49:10 pia soma. 2Samweli 7:16-17

4. Je Daudi alipakwa mafuta mara ngapi na wapi?

Jibu. Mara tatu

=Mara ya kwanza Bethlehemu (nyumbani kwa Yese) 1samweli 16:12-13

=Mara ya pili Hebroni kuwa mfalme wa Yuda 2samweli 2:3-4

=Mara ya tatu Hebron kuwa mfalme wa Israeli. Soma 2Samweli 5:2-4

5. Je ni mji gani ambao Barnaba na Paulo waliwekewa mikono na kanisa kwa agizo la Bwana?

Jibu. ANTIOKIA

Soma. Matendo ya mitume 13:1-3

6. Ni mfalme gani aliye tumia vyombo vya hekaluni kwa anasa Mungu akamwadhibu siku hiyo hiyo?

Jibu. BELSHAZA (mfalme wa Babeli)

Soma. Danieli 5:1-31

7. Je ni nabii gani aliye tabiri kutoroka kwa mfalme Sedekia kwa kuuvunja ukuta wa yerusalemu kisha kukamatwa na kupelekwa babeli?

Jibu. NABII EZEKIELI

Soma. Ezekieli 12:1-13

8. Ni nabii gani aliye tabiri kukamatwa kwa paulo na kufungwa miguu na mikono?



Jibu. NABII AGABO

Soma. Matendo ya mitume 21:10-13

9. Je ni Nabii gani aliye tabiri (wakati wa kanisa la kwanza la mitume) ujio wa njaa kubwa kutokea katika dunia nzima katika siku za Klaudio.

Jibu. NABII AGABO

Soma. Matendo ya mitume 11:28

10. Je ni nani aliye itabiria Yuda kuwa yeyote atakaye baki hapo Yuda atakufa kwa makali ya upanga na kwa njaa, bali atakaye toka kumtumikia mfalme wa Babeli ataishi?

Jibu. NABII YEREMIA

Soma. Yeremia 21:1-10

BWANA YESU akubariki Mjoli wa BWANA.

@NURU YA UPENDO

www.wingulamashahidi.org

0652274252 au 0693036618